

HOMA YA NGURUWE INAVYODIDIMIZA UCHUMI WA WANANCHI.

Noah Kibona, Rungwe DC

Mtaalamu wa mifugo kanda ya Iringa Dr. Solomon Nog'ona anataja idadi ya nguruwe wanaofugwa nchini Tanzania kuwa wanakadiliwa kufikia million 2.14 na asilimia 60% ya nguruwe hao hufugwa mikoa ya Nyanda za juu kusini ambapo kwa mwaka huzalisha faida inayokadiriwa kufikia billion 250.

Mkurugenzi wa huduma ya mifugo kutoka wizara ya Mifugo na uvuvi Profesa Hezron Nonga anazitaja faida za ugugaji wa nguruwe kuwa ni pamoja na kuongeza lishe kwa ngazi ya kaya, kipato kwa jamii na mbolea katika mashamba ya wakulima.

Mwaka 2010 ulikuwa mwaka usio na neema kwa wakazi wa nyanda za juu kusini. Wimbi kubwa la nguruwe liliteketea. Haikuwa sababu nyingine bali ni ugonjwa wa homa ya nguruwe (**African swine fever**) ambapo tangu uingie nchini kupitia mlango wa nchi ya Malawi wilaya ya Kyela katika mkoa wa Mbeya umerudisha sana juhudi za wafugaji wa Nguruwe.

Ugonjwa huu unaolipuka zaidi kuanzia mwezi **November- Februari** husababishwa na virusi ambavyo huambukiza kwa haraka sana kutoka nguruwe pori na kwenda kwa nguruwe wanaofugwa ambao hatimae huenezwa na nguruwe wenyewe kwa wenyewe wanaofugwa kwa kugusana. Mpaka sasa ugonjwa huu haujatokomezwa pamoja na juhudi nyingi za serikali na wadau wa sekta ya mifugo unaoendelea. anafafanua Profesa Gerald Misinzo kutoka chuo kikuu cha kilimo "SUA" Mkoani Morogoro.

Ugonjwa huu umeenea nchi nzima huku mikoa ya nyanda za juu kusini ikiwa na maambukizi ya juu zaidi kwa asilimia 60%. Awali uligundulika nchini Kenya mwaka 2010 na kwa sasa umeenea dunia nzima huku nchi ya China barani Asia ikiongoza kwa maambukizi.

Ayubu Mwakamela ni mfugaji wa kata ya Matwebe wilaya ya Rungwe, na anautaja ugonjwa huu kama mshale wenye sumu katika harakati zake za kujikwamua kiuchumi kwani mwaka 2011 takribani nguruwe wake 10 walikufa kutokana na ugonjwa huu. Kwa wakati ule hakuwa na uelewa mpana na namna ya kukabiliana na kusambaa kwake lakini kwa sasa baada ya msaada mkubwa kutoka kwa wataalamu wa mifugo anaweza kupambana na madhila yake.

Hali imekuwa tofauti kwa Kefa Mwakisambwe mkazi wa kata ya Kiwira kwani yeye ameamua kufuga kuku na samaki baada ya kuteketeza nguruwe wapatao 20 kutokana na kukosa ujuzi wa kupambana na ugonjwa huu.

Lakini Ayubu Mwakisu hajapata madhara yeyote toka ugonjwa huu uingie nchini kwa kuwa yeye tayari ametengeneza mazingira ya mifugo yake kutoingiliana na mifugo toka nje ya himaya yake ikiwa ni pamoja na kutumia viuawadudu mara kwa mara.

DALILI ZA HOMA YA NGURUWE

1. Nguruwe hunyong'onyea na kukosa hamu ya kula na kukusanyika mahali pamoja.
2. Joto kali la mwili huongezeka mpaka kufikia nyuzi 42 C
3. Nguruwe huwa na rangi ya bluu au nyekundu katika sehemu za mwili hasa zisizo na manyoya marefu kwenye masikio, nyuma na mapaja, chini ya tumbo na miguu.
4. Nguruwe hutoa kinyesi chenye damu na kushindwa kusimama.
5. Kutapika, kuharisha na kupungua uzito.
6. Kutupa mimba na vifo hutokea baada ya wiki moja au mbili.
7. Ukipasua ndani utakuta kongosho, figo, na viungo vingine vikiwa vimevimba na kujaa damu.

UENEAJI WA UGOJWA HUU

Ugonjwa huu husambaa zaidi kuanzia mwezi wa **novemba mpaka Februari** na husambaa kupitia kupe laini (Ornithodoros) mwenye vimelea kwa kunyonya damu ya nguruwe asiye na ugonjwa. Pia ugonjwa husambaa kwa njia ya majimaji au damu ya nguruwe mgonjwa. Ugonjwa huu pia unaweza kuenea kwa njia hizi:

1. Utupaji wa nguruwe waliokufa na homa ya nguruwe hovyoyovyoyo au katika vyanzo vya maji.
2. Kuingiza nyama au nguruwe kutoka nchi jirani bila kuzingatia taratibu za idara ya mifugo.
3. Ununuzi wa nguruwe hasa katika meneo ambayo ugonjwa tayari umebainika kuwepo. Tabia ya kununua nguruwe kutoka kona moja hadi nyingine ni vema ukapata ushauri au kibali kwa afisa mifugo.
4. Ufugaji huria au kuruhusu wafugaji kuingia katika banda la nguruwe bila kuchukua tahadhali zinazostahili.

KWA NINI UGONJWA HUU HUENEA WAKATI WA MVUA.

Ugonjwa huu huenea zaidi wakati wa mvua kwa kuwa wakati huo mvua huchagiza utiririshaji wa maji kutoka eneo moja hadi lingine. Maji ya mvua hubeba kinyesi cha nguruwe, mikojo, mizoga, bakteria kutoka eneo lililoathirika hadi lingine. Pia wakati huo mazalia ya wadudu yanaongezeka kwa kasi hali inayopelekea ndege hasa kuku kuparua kando na ndani ya banda na hivyo kubeba vimelea katika mabawa na miguuni na kuyasambaza maeneo mengine.

VIFO VYA NGURUWE WILAYANI RUNGWE KUTOKANA NA HOMA YA NGURUWE

Dr. Israel Mwalyaje ni mtaalamu wa mifugo halmashauri ya wilaya ya Rungwe na avitaja vifo vya nguruwe kuwa ni pigo la kipato kwa wafugaji anaowasimamia. Mathalani nguruwe mmoja wa

umri wa kuchinjwa huuzwa kwa wastani wa shilingi 150,000 hadi 350,000/= hivyo mwaka 2010 pato la mauzo ya nguruwe linalokadiriwa kufikia 127,000,000 lilipotea. Lakini elimu pamoja juhudi za maafisa ugani kuwatembelea wafugaji katika kaya zao vifo vimemeendelea kushuka kama jedwali linavyoonesha chini.

| S/N | MWAKA | IDADI YA NGURUWE WALIOKUFA KIWILAYA | IDADI YA NGURUWE KIWILAYA |
|------------|--------------|--|----------------------------------|
| 1 | 2010 | 635 | 56,876 |
| 2 | 2011 | 493 | 56,241 |
| 3 | 2012 | 459 | 55,782 |
| 4 | 2013 | 315 | 26,467 |
| 5 | 2014 | 07 | 18,922 |
| 6 | 2015 | 0 | 21,234 |
| 7 | 2016 | 0 | 22,311 |
| 8 | 2017 | 15 | 23,309 |
| 9 | 2018 | 5 | 24,495 |
| 10 | 2019 | 68 | 16,510 |

MADHARA YA HOMA YA NGURUWE

Ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo na unapointia katika banda la mfugaji nguruwe wengi huugua na kufikia asilimia 100. Kwa hiyo ugonjwa huu husabababisha kutokuwa na usalama wa chakula na kuleta umasikini. Aidha wananchi wa kipato cha chini na kwa kiasi kikubwa wanashindwa kutatua mahitaji kama vile ada ya shule, matibabu na huduma za fedha vijijini (Village cooperatives Bank-VICOBA)

NAMNA YA KUTHIBITI HOMA YA NGURUWE

Mtalaamu wa mifugo Dr. Mwalayaje anazitaja mbinu ambazo wakulima wanaweza kuzitumia ili kuondokana na vifo vya nguruwe na hivyo kupandisha kipato cha kaya na taifa kwa ujumla.

1. Mara vifo vinapotokea au dalili kubainika toa taarifa kwa mtaalamu wa mifugo
2. Pulizia dawa za kua vidudu ndani na nje ya banda la nguruwe mara moja kwa mwezi ikiwa ni pamoja na kufanya usafi mara kwa mara.
3. Nunua nguruwe au Nyama yake katika maeneo ambayo yamehakikiwa kuwa hayana maambukizi ya homa ya nguruwe.
4. Vyombo vya usafiri kama Magari, matrekta, guta au pikipiki vipuliziwe dawa kabla na baada ya kupakia nguruwe .
5. Tengeneza sehemu ya kuweka dawa ya kukanyaga wakati unaingia na kutoka kwenye banda.
6. Watu kando na mhudumu wasikaribie au kuingia katika banda la nguruwe.
7. Usichanganye nguruwe wenyeji na wageni.
8. Chakula cha nguruwe kinunuliwe maeneo ambayo ugonjwa umeripotiwa.

WAMILIKI WA BUCHA WAONYWA

Mtalaanu kutoka shirika la chakula Duniani “FAO” Profesa Folorunso Fasina anawanyoshea kidole wachinjaji na wamiliki wa maduka ya kuuzia nyama ya nguruwe kuwa ni kikwazo cha juhudi za kutokomeza ugonjwa huu kwani wamekuwa wakinunua nguruwe wagonjwa kwa bei nafuu na kuuza nyama kwa bei kubwa na kupata faida lukuki huku wakiendelea kusambaza ugonjwa kwa wanunuzi kula nyama na kusambaza mabaki ovyo.

FAIDA YA UFUGAJI WA NGURUWE

Mfugaji kutoka chama cha wafugaji wa Nguruwe “TAPIFA” bibi Doreen Maro anazitaja faida za ufugaji wa nguruwe kuwa ni pamoja na:

1. Nguruwe huongeza kipato cha kaya kwani kitoto cha nguruwe huuzwa kati ya shilingi 50,000/= hadi 60,000/= kwa mbegu ya kawaida. Lakini hufikia hadi 80,000/= kulingana na aina ya mbegu. Nguruwe anaweza kuzaa watoto hadi kufikia 18 kutokana na lishe, aina ya mbegu, matibabu na huzaa mara mbili hadi nne kwa mwaka. Hali hii inaweza kumkwamua mfugaji kwa kujenga nyumba ya kisasa, karo kwa watoto shuleni, kulipia ankara mbalimbali kama maji, umeme, nauli, utalii na matibabu.

2. Nguruwe husaidia upatikanaji wa mbolea kwa ajili ya kilimo cha mazao ya bustani na mazao mengine ya kudumu.

3. Nguruwe wameongeza ajira kwa wananchi wengi kufungua maduka ya kuuza nyama ya nguruwe, kusafirisha nguruwe na maduka ya kuuza vyakula vya mifugo.

